TGNP

# Utengaji Rasilimali kwa ajili ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Nchini Tanzania



## Uchambuzi wa Bajeti Kijinsia

Sweden Sverige

TGNP

In partnership with Canada



# Utengaji Rasilimali kwa ajili ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Nchini Tanzania

## Uchambuzi wa Bajeti Kijinsia

# CONTENTS

Utangulizi ..... 1
Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Nchini Tanzania (MTAKUWWA)..... 2
Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa MTAKUWWA ..... 3
Mwaka wa Kwanza wa MTAKUWWA ..... 4
Mwaka wa Pili wa MTAKUWWA ..... 5
Mwaka wa Tatu wa MTAKUWWA ..... 6
Mwaka wa Nne wa MTAKUWWA..... 7
Mwaka wa Tano wa MTAKUWWA ..... 8
Mapungufu Yaliyoainishwa ..... 9
Hitimisho na Mapendekezo ..... 10

## Utangulizi

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni changamoto kubwa inayoikumba dunia na inayoathiri makundi mbalimbali ya watu katika jamii. Licha ya ukatili huo kumwathiri kila mtu, wanawake na watoto ni kundi linaloathirika zaidi kwa sababu, kwa bahati mbaya, haki zao zinakandamizwa au wanakosa utetezi sahihi dhidi ya ukatili huu. Katika baadhi ya jamii, aina fulani za ukatili huchukuliwa kuwa sehemu utamaduni wa jamii hizo; na aina hizo za ukatili zinakubalika kijamii na kisheria. Matokeo yake, wanawake na watoto wanaendelea kupata madhara. Kiasi cha 98% ya wanaoathiriwa na ukatili wa kingono ulimwenguni ni wanawake huku 55% wamo katika ajira hatarishi. Aidha, 35% ya wanawake hukumbana na ukatili wa kimwili au wa kingono katika maisha yao huku zaidi ya wasichana milioni 250 waliovunja ungo hulazimishwa kuolewa.

Nchini Tanzania, takwimu[1] zinaonesha kuwa na idadi kubwa ya ukatili wa kimwili au kingono (46.2%), ndoa za utotoni, za umri wa mapema na za kulazimishwa (30.5%), ukeketaji (10%), na 33.3% ya wasichana hukumbana na ukatili wa kingono kabla ya kufikia umri wa utu uzima kwa wale waliohojiwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, asilimia tisa ya wanawake walio kati ya miaka 15-49 hukumbana na ukatili wa kingono[2], na 3.5% na 18% ya wasichana huolewa kabla ya kufikia miaka 15 na 18. Kwa mwaka 2017/18 pekee, jumla ya matukio 1,091 ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yaliripotiwa katika vituo vya polisi, na kati ya hayo, waathirika 945 (87%) walikuwa watoto na 146 (13%) wanawake.

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto uhusishwa moja kwa moja na mifumo iliyopo pamoja na mitazamo inayojengwa na mfumo dume ambayo inachangia kukosekana kwa usawa kati ya wanawake na wanaume. Hivyo, Tanzania imeorodheshwa katika nafasi ya 140 na 82 katika kipimo cha Usawa wa Kijinsia na kile cha Pengo la Jinsia, mtawalia. Kwa mujibu wa Taasisi za Kijamii za OECD na kipimo cha Usawa Kijinsia, suala la ukatili dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa zaidi upande wa Tanzania Bara (kwa alama 39) kuliko Zanzibar (kwa alama 25).

Bila kujali sababu za kimazingira, ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaigharimu jamii kiafya na kiuchumi. Jamii hulazimika kulipia gharama za ukatili kupitia mifumo ya afya, unasihi na huduma nyingine zinazohusiana na hizo, mifumo ya utoaji haki, utoaji huduma za usaidizi kwa watoto na ustawi wa jamii, pamoja na gharama zisizo za moja kwa moja kama vile kupoteza kipato, kudhoofisha uzalishaji na kudidimiza satua. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN Women), gharama zinazosababishwa na ukatili dhidi ya wanawake na watoto hufikia asilimia mbili ya pato la taifa. Katika kuangazia masuala ya kimataifa, ukatili dhidi ya wanawake na watoto umetajwa kuwa miongoni mwa vikwazo vya kutimiza mipango ya maendeleo endelevu. Vilevile, Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu imejumuisha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika orodha ya vipaumbele na malengo yaliyo chini ya Lengo Namba tano linalohusu usawa wa kijinsia.

## Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Nchini Tanzania (MTAKUWWA)

Pamoja na ajenda za kimataifa na kikanda kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake, na kwa kuongozwa na mikataba iliyoridhiwa katika itifaki mbalimbali za kimataifa, kikanda na ujirani, Tanzania imekuwa nchi ya kipaumbele katika kushughulikia masuala ya

1 Tazama Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey [TDHS-MIS] 2015-16. Dar es Salaam, Tanzania, na Rockville, Maryland, 2016.
2 TDHS-MIS 2015-16

ukatili katika ukanda huu. Mwaka 2009, Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kufanya utafiti kuhusu ukatili dhidi ya watoto (wenye umri kati ya 13-24) uliolenga kupima kuwapo kwa ukatili wa kihisia, kimwili na kingono. Kuzinduliwa na kufanyika kwa utafiti huu mwaka 2011 ilikuwa ishara kubwa inayoonesha nia ya dhati ya serikali ya kukabiliana na kutokomeza ukatili dhidi ya watoto kama suala la dharura na la haraka.[3]

Hatimaye, Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 - 2021/22) ulianza kutumika mwezi Disemba 2016, suala lililoifanya Tanzania kupata hadhi na kuingia katika kundi la nchi za kipaumbele katika Ushirikiano wa Kimataifa unaolenga Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. MTAKUWWA unaweza kutazamwa kama kichocheo muhimu katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jinsia ya mwaka 2020, inayolenga kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili kuboresha ustawi wao.

Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto wa miaka mitano (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22) uliandaliwa kwa kuileta pamoja mipango kazi minane iliyokuwapo tayari ambayo ilikuwa ikishughulikia suala la ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini. MTAKUWWA umejikita katika kusisitiza hatua zinazohitajika katika uandaaji wa mikakati ya kuzuia na kushughulikia matukio ya ukatili kwa sababu mikakati hiyo ina mchango chanya katika kuleta ustawi jumuishi. Ili kufikia malengo ya MTAKUWWA, rasilimali zinahitajika kutoka kwa serikali na wadau mbalimbali.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kiasi cha bajeti ambacho kimekuwa kikitengwa kwa ajili ya matumizi ya umma, hususan kinacholenga sekta ya afya kimekuwa kikishuka. Pamoja na matumizi katika sekta ya afya katika kipindi cha kati ya mwaka wa fedha wa 2013/2014 na wa 2017/2018 kuendelea kuwa chini ya lengo lililowekwa katika Makubaliano ya Abuja ya kutenga 15%, kiasi hicho kilishuka zaidi kutoka 9.6% hadi 7.0%. Katika takwimu za kitaifa za upelekaji wa fedha, inaoneshwa kuwa si rahisi kufuatilia mwenendo wa upelekaji wa fedha kwa sababu ucheleweshaji na upelekaji wa fedha hutokea katika ngazi ya wizara na katika serikali za mitaa[4]. Katika mwaka wa fedha wa 2016/17, 25.8% tu ya kiasi cha fedha kilichopitishwa, yaani takribani Sh. bilioni 518.5, na fedha hizo zilifika katika taasisi na mashirika husika ndani ya wizara[5] baada ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Utekelezaji wa bajeti umeendelea kuwa tatizo la sugu na la kudumu, hususani pale ambapo fedha hazitolewi kwa wakati.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni taasisi inayoshughulikia harakati katika masuala ya kijamii, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. TGNP imekuwa mstari wa mbele katika kuibua na kusimamia mikakati mbalimbali inayolenga kujumuisha masuala ya kijinsia katika miongozo na mikakati ya kitaifa. Vilevile, imefungua njia ya kuhakikisha kuwa bajeti zinazingatia mahitaji ya jinsia katika wilaya teule za mfano nchini Tanzania kwa kushirikiana na wafadhili ili kuisaidia serikali kukuza usawa wa kijinsia. Pia, TGNP ina mchango na nafasi kubwa katika MTAKUWWA – jambo linaloufanya uchambuzi huu wa kifedha wa utekelezaji wa mpango kazi huu wa MTAKUWWA kuendana na dira ya TGNP ya kuainisha mapungufu na ushahidi utakaowezesha uchechemuzi na utetezi wa ziada unaolenga kutokomeza ukatili na kuboresha ustawi.

3 Together for Girls [TfG] [2018], Accelerating Action to Address Violence Against Women and Children: key lessons from the Together for Girls partnership in Tanzania

4 Madaha, R. M. [2018]. Budget Analysis and Tracking on GBV financing: The Case of Selected Government Ministries in Tanzania, http://www.emeraldinsight.com/doi/abs/10.1108/17595901211263675

5 SIKIKA [2017], Health Sector Budget Analysis for fiscal year 2017/2018. Policy Brief

## Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa MTAKUWWA

Mwanzoni mwa utekelezaji wa MTAKUWWA, serikali ilibainisha gharama za utekelezaji wa mpango huu kuwa Sh. bilioni 267.4 katika kipindi cha miaka mitano zikiwa zinalenga afua za kuzuia na kushughulikia matukio ya ukatili kama ilivyoainishwa katika maeneo makuu manane ya mkakati huu. Kwa mujibu wa MTAKUWWA, makisio ya gharama za matumizi ya kawaida yalikuwa Sh. bilioni 247.4 na mtaji Sh. bilioni 20.0. Serikali ililenga kutafuta fedha hizo kupitia vyanzo mbalimbali, vya umma na binafsi; na kisha kutenga bajeti katika malengo na afua za kimkakati.

Kwa mujibu wa MTAKUWWA, makisio ya gharama za matumizi ya kawaida yalikuwa Sh. bilioni 247.4 na mtaji Sh. bilioni 20.0

Kushughulikia mila kunaoneshwa kuwa zaidi **(36.5%)**

Kuimarisha kaya kiuchumi **(22.8%)**

**Takwimu zinaonesha jumla ya bajeti iliyotengwa kufadhili mikakati ya MTAKUWWA katika kipindi cha miaka mitatu ni Sh. bilioni 24.9.**

| Wizara, Idara na Taasisi | Serikali za Mitaa | Wachangiaji wengine, zikiwemo AZAKI na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali | Wahisani |
|---|---|---|---|
| **(Sh. bilioni 12.6)** | **(Sh. bilioni 6.8)** | **(Sh. bilioni 4.1)** | **(Sh. bilioni 1.4)** |

MTAKUWWA umetambua mchango wa wadau nje ya serikali na kuainisha mchango wao katika kufadhili mikakati mbalimbali. Uchambuzi huu umebaini kuwa ushiriki umetofautiana kwa kiasi kikubwa, hususani baina ya Wadau wa Maendeleo na AZAKI za ndani. Hata hivyo, tunawapongeza na kuwatambua wote waliochangia. Taasisi za UNICEF, UN Women, Women Fund, UNFPA, Umoja wa Ulaya, na Balozi za Ufaransa, Kanada, Uholanzi, na Uswidi zilikuwa miongoni mwa wadau wa maendeleo waliokuwa wakiwezesha MTAKUWWA. UNICEF na Umoja wa Ulaya wamekuwa wadau muhimu katika kutoa mchango wa kifedha na kiutendaji katika eneo la Utekelezaji na Usimamizi wa Sheria, hasa katika eneo la uimarishaji wa miundombinu ya Mtandao wa Madawati ya Jinsia, Wanawake na Watoto katika ngazi za Polisi na Jamii.[6] Aidha, UNFPA wametoa mchango mkubwa katika maeneo mengine mawili yahusuyo Mila na Desturi pamoja na Utoaji wa Huduma kwa Waathirika wa Ukatili.

Jumla ya Asasi za Kiraia (AZAKI) 1,801 zilijihusisha na utekelezaji wa afua zihusuzo "Mila na Desturi" katika MTAKUWWA. Michango ya AZAKI imekwamishwa na sababu mbalimbali zikiwemo kukosa fedha na kutegemea wahisani, pamoja na sababu nyinginezo.

6 Tanzania Daily News, "Tanzania: How Police Gender, Children's Desk Help Community," 6 January 2021, at https://allafrica.com/stories/202101060051.html


## Mwaka wa Kwanza wa MTAKUWWA

Katika kipindi cha 2017/2018, mwaka wa kwanza wa fedha wa utekelezaji wa MTAKUWWA, serikali ililenga kutumia Sh. 29,376,194,500. Mwongozo wa bajeti wa 2017/2018 ulishindwa kuratibu na kutoa maelekezo kwa wizara ijumuishe mikakati ya MTAKUWWA katika bajeti zao. Mwongozo huo ulitoa maelekezo kwa wizara ya kuzingatia masuala ya jinsia pekee na si ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto kama miongoni mwa masuala mtambuka. Hata hivyo, mwongozo hauoneshi hatua mahususi zinazolenga kushughulikia ukatili dhidi ya wanawake na watoto kama ilivyoainishwa katika malengo mahususi yaliyopo kwenye MTAKUWWA.

Katika eneo la kuimarisha uchumi wa kaya, MTAKUWWA ulilenga kuongeza idadi ya wanawake wanaofikia huduma za kifedha kutoka 51.2% mwaka 2016 hadi 65% mwaka 2021/22. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJJWW), chini ya fungu dogo la bajeti namba 3001, haikutenga fedha za uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 (JMT, 2017). Sababu za kutofautiana huku hazipo bayana, kwani serikali ilipitisha Sh. 1,955,000,000 kwa ajili ya uwezeshaji kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2016/17 (JMT, 2017).

Vilevile, MTAKUWWA ulilenga kuongeza idadi ya vikundi vya wanawake vilivyofuzu na kuingia katika vyama vya akiba na mikopo - SACCOS kutoka asilimia moja hadi 15% na vilevile kuongeza idadi ya wanawake wanachama wa VICOBA kutoka 79% hadi 85%. Malengo haya hayakuwepo katika mwongozo wa bajeti wa mwaka wa fedha 2017/2018 wala mikakati ya kuyafikia haikuelezwa kwa uwazi katika bajeti ya WAMJJWW na katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI).

Bajeti ya OWM – TAMISEMI haikuupa kipaumbele MTAKUWWA wala kushawishi utekelezaji wake kama ilivyoainishwa katika MTAKUWWA. Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya 2017/2018 haioneshi uanzishwaji wa kamati ya pamoja ya uratibu, usimamizi na ufuatiliaji ndani ya wizara hiyo, hasa bajeti ya maendeleo ya OWM – TAMISEMI inajumuisha programu ya ushindani kwa sekta binafsi (Sh. 16,258,594,844), ujenzi wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sh. 5,000,000,000) na uratibu wa shughuli za serikali kupitia MIVARF5 (Sh. 43,145,159,919).




*Katika eneo la kuimarisha uchumi wa kaya, MTAKUWWA ulilenga kuongeza idadi ya wanawake waliopata huduma za kifedha kutoka 51.2% mwaka 2016 hadi kufikia 65% mwaka 2021/22, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (WAMJJWW), chini ya fungu dogo la bajeti namba 3001, haikutenga fedha za uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 (JMT, 2017).*

## Mwaka wa Pili wa MTAKUWWA

Katika Mwongozo wa Bajeti ya Taifa wa mwaka wa fedha wa 2018/19, maeneo ya kipaumbele na miradi iliyopangwa kutekelezwa ilitokana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Pili. Vipaumbele hivyo vilijumuisha afya na elimu. Hata hivyo, mwongozo haukusema chochote kuhusu kujumuisha MTAKUWWA. Katika kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/19, bajeti ya serikali iliweka msisitizo katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na afua zilizolenga kuboresha maendeleo ya watu na kujenga mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara. Serikali ilitenga jumla ya Sh. bilioni 978.4 ili kuwezesha makundi mbalimbali kushirikiana katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Katika hifadhi ya jamii, eneo kubwa la matumizi lilikuwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii (Sh. bilioni 946.2), na Sh. bilioni 1.8 kwa ulinzi wa watoto. Uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2018/19[7] unaonesha kwamba 'sekta' ya hifadhi ya jamii ilinufaika kwa 22% pekee. Utekelezaji huu hafifu una athari mbaya katika kufadhili shughuli za MTAKUWWA, hasa katika ngazi ya serikali za mitaa. Utafiti mmoja[8] unaonesha bajeti inayotengwa kwa Jeshi la Polisi ni ndogo sana katika kutekeleza shughuli za MTAKUWWA, matokeo yake, fedha hizo huelekezwa katika matumizi mengine ya msingi kama vile bili za maji na umeme. Kwa mfano, utafiti huo unaonesha kuwa, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, mahitaji halisi ya fedha yalikuwa Sh. 200,1500,200 lakini ni asilimia tano pekee ya kiasi hicho cha fedha ndiyo ilipelekwa katika taasisi hiyo. Hali hiyo iliathiri moja kwa moja ufanisi wa Madawati ya Jinsia na Watoto ya Jeshi la Polisi.

Wadau wa Maendeleo, na hasa UNICEF, Umoja wa Ulaya na UNFPA wamekuwa wadau muhimu katika kutoa msaada wa kifedha na kiutendaji kwa madawati ya jinsia na watoto kote nchini. Kwa kuwa fedha za wahisani hazitabiriki, hakuna uhakika wa moja kwa moja kwa wanawake na wasichana kuzifikia huduma hizo muhimu zinazotolewa na madawati ya jinsia na watoto, zikijumuisha fomu maalumu za kupatiwa huduma za afya na uchunguzi (PF3), ukamatwaji wa watuhumiwa, kufungua kesi, ukusanyaji wa ushahidi na vielelezo, uchunguzi na kutembelea eneo la tukio na pia kupeleka jalada kwa wakili, na hatimaye, mahakamani. Kutokana na changamaoto hiyo, mafanikio ya madawati haya yameripotiwa kutofautiana. Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari[9], kutokana na kukosekana fedha za kutosha, madawati ya jinsia 30 pekee yalifanikiwa kuanzishwa kati ya madawati 417 kwa mujibu wa mwongozo wa vigezo.

7 MoFP [2019], The Budget Execution Report for the Third Quarter of 2018/19. Dodoma, p.16

8 Mlay, Berthaneema W. [2020]. "Implementation of National Plan of Action to end Violence against Women and Children: A Case of Tanzania Police Force," Dar es Salaam: Mzumbe University

9 Tanzania Daily News, "Tanzania: How Police Gender, Children's Desk Help Community," 6 January 2021, at https://allafrica.com/stories/202101060051.html

*katika mwaka wa fedha wa* **2018/19,** *mahitaji halisi ya fedha yalikuwa Sh.* **200,150,200**



*Kwa mfano, utafiti huo unaonesha kuwa katika mwaka wa fedha wa 2018/19, mahitaji halisi ya fedha yalikuwa Sh. 200,150,200 lakini ni asilimia tano pekee ya kiasi hicho cha fedha ndiyo ilipelekwa. Hali hiyo iliathiri moja kwa moja ufanisi wa madawati ya jinsia na watoto la Jeshi la Polisi.*

## Mwaka wa Tatu wa MTAKUWWA

Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2019/20 ilijikita katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17-2020/21 uliokuwa na kaulimbiu ya "kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii". Ili kufikia malengo haya ya ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii yalitengewa jumla ya Sh. bilioni 47.0 kwa mwaka wa 2019/20 ili kuboresha huduma na maendeleo ya jamii.

Miongoni mwa maeneo manane yaliyoainishwa katika maendeleo ya jamii, serikali ilitenga Sh. bilioni 3.4 kwa ajili ya uratibu wa utekelezaji wa MTAKUWA, na nyongeza ya Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya kuchagiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi, kusambaza teknolojia stahiki kwa wanawake wajasiriamali, uratibu wa shughuli za kifedha kwa vikundi vya wanawake, SACCOS na VICOBA. Hata hivyo, uchambuzi wa takwimu za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 uligundua kuwa MTAKUWWA haukuwepo kwenye orodha ya vipaumbele kimatumizi katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka kwa mwaka wa fedha wa 2019/20.

Kwa mujibu wa serikali, utekelezaji wa bajeti ulio chini ya kiwango tarajiwa kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 ulisababishwa na mapato hafifu katika baadhi ya vyanzo vya ndani na vile vya nje uliochangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za janga la UVIKO-19. Uchambuzi wa kijinsia umegundua kuwa tatizo kubwa lilikuwa suala la kupanga vipaumbele na si upatikanaji wa fedha. Kwa mfano, katika sekta ya elimu, mipango ya matumizi kwa programu, miradi na shughuli mbalimbali haikulitilia maanani kabisa eneo la "Shule Salama na Stadi za Maisha" lililopo kwenye MTAKUWWA licha ya Wizara ya Elimu kupangiwa utekelezaji wa eneo hilo. Badala yake, maeneo makubwa ya kimatumizi yalikuwa Elimu ya Msingi bila Ada (Sh. bilioni 288.4); miundombinu ya shule za msingi na sekondari (Sh. bilioni 165.62); mitihani ya taifa (Sh. bilioni 73.97); mafunzo ya ufundi (Sh. bilioni 62.94): sayansi, teknolojia, ubunifu, tafiti na maendeleo (Sh. bilioni 75.35); mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu (Sh. bilioni 450.00) na ubora wa elimu kupitia taasisi za ukaguzi (Sh. bilioni 218.38).

Ingawa haya yote ni maeneo muhimu yanayolenga kusaidia kushughulikia mahitaji ya kimkakati ya kijinsia ya wanawake na wasichana, kwa wasichana na wavulana wanaolengwa, jambo hili lingefanikiwa zaidi ikiwa wangelindwa zaidi kupitia utoaji nasaha na mwongozo kwa waalimu juu ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Aidha, suala hili lingesaidia kuongeza uelewa kwa walengwa kuhusu namna ya kutoa ripoti za ukatili shuleni – kama ilivyobainishwa katika MTAKUWWA.

*Kwa mujibu wa serikali, utekelezaji wa bajeti ulio chini ya kiwango tarajiwa kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 ulisababishwa na mapato hafifu kwa baadhi ya vyanzo vya ndani na vile vya nje uliochangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za janga la UVIKO-19. Uchambuzi wa kijinsia umegundua kuwa tatizo kubwa lilitokana na upangaji wa vipaumbele na si upatikanaji wa fedha.*

## Mwaka wa Nne wa MTAKUWWA

Katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2020/21, mwongozo wa bajeti ulielekeza kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti, na kwamba "Wahasibu wanatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mtambuka yakiwemo yale yahusuyo jinsia".[10] Kuzingatia jinsia pekee hakujapewa umuhimu na msisistizo kama ilivyo kwa NACSAP III, Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Umma Awamu ya III, na Programu ya Mageuzi ya Serikali za Mitaa Awamu ya III, kama inavyobainishwa katika mwongozo.

Kwa mujibu wa ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2020/21, kiasi cha fedha zilizopelekwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo hadi kufikia robo tatu ya mwaka wa fedha kufikia Sh. bilioni 2,822.2, sawa na 88.3% ya kiasi kilichopangwa cha Sh. bilioni 3,194.8, ambapo ni 47.2% zaidi ya kiasi kilichopelekwa 2019/20. Kwa ujumla, huu ni mwelekeo chanya.

Mnamo tarehe 31 Machi 2020, Benki ya Dunia iliidhinisha mkopo wa thamani ya dola za Kimarekani milioni 500 kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kufadhili Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP). Mradi huo unalenga kuweka mazingira salama na bora ya kujifunzia kupitia kifungu cha tatu – Kupunguza Vikwazo vya Kielimu kwa Wasichana kwa Kurahisisha Ufikiwaji wa Elimu ya Sekondari)[11]. Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilipewa jukumu la kusimamia ujenzi wa Programu ya Shule Salama iliyolenga kuhakikisha kuwapo kwa shule salama zinazozingatia mahitaji ya jinsia na mazingira rafiki kwa wanaojifunza. Programu hii, iliyo chini ya MTAKUWWA, ilitengewa bajeti ya kiasi cha dola za Kimarekani milioni 180, ambapo bajeti iliyotengwa kwa Shule Salama na Stadi za Maisha kutoka mwaka wa fedha wa 2020/21 – 2021/22 ilikuwa Sh. 16,757,860,160.

Ni dhahiri kuwa MTAKUWWA umepewa kipaumbele kidogo katika mchakato wa bajeti kwa sababu katika miaka ya hivi karibuni, serikali ilijikita zaidi kuhakikisha bajeti ya nchi inategemea zaidi mapato ya ndani huku ikipunguza utegemezi wa michango ya wahisani kutoka zaidi ya 70% hadi kufikia chini ya 40% hivi sasa. Katika kuufadhili MTAKUWWA, serikali imekuwa ikitegemea zaidi fedha za wahisani ambapo utoaji wao wa fedha hautabiriki.

*Kwa mujibu wa ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2020/21, kiasi cha fedha zilizopelekwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo hadi kufikia robo tatu ya mwaka wa fedha, kilifikia Sh. bilioni 2,822.2, sawa na 88.3% ya kiasi kilichopangwa cha Sh. bilioni 3,194.8, ambapo ni 47.2% zaidi ya kiasi kilichopelekwa 2019/20. Kwa ujumla, huu ni mwelekeo chanya.*

10 MoFP [2019], Guidelines for Preparation of Plans and Budget 2020/21. Dodoma: MoFP, p.49

11 World Bank [2020], "New Financing to Make Secondary Education Safer, Better, and More Accessible for Tanzanian Girls and Boys", Press Release No: 2020/021/AFR.

## Mwaka wa Tano wa MTAKUWWA

MTAKUWWA ulitengewa Sh. 34,549,608,080 kwa mwaka wa fedha wa 2021/22. Maeneo yaliyozingatiwa zaidi yalikuwa kuboresha kaya, mila na desturi pamoja na Program ya Shule salama na stadi za Maisha. Kwa mujibu wa mwongozo wa bajeti wa mwaka wa fedha 2021/22, pato la taifa lilitegemewa kuongezeka kutoka 5.0% hadi 5.2%, ambapo matumizi makubwa yalielekezwa katika miradi ya kimkakati na sensa lakini hakuna fedha maalum zilizotengwa kwa afua za MTAKUWWA au maeneo yake na kuripotiwa na serikali kama ilivyoainishwa hapa chini kwa sekta nyingine.

Sekta tatu za ustawi wa jamii ambazo zinahusiana moja kwa moja na MTAKUWWA zilijumuishwa katika vipaumbele hivyo ambavyo ni afya, hifadhi ya jamii na usimamizi na utekelezaji wa sheria. Matumizi ya sekta hizi zote yalitarajiwa kuongezeka: kutoka Sh. bilioni 2,019.2 hadi Sh. bilioni 2,188.9 (afya), kutoka Sh. bilioni 1,853.4 hadi Sh. bilioni 2,009.2 (hifadhi ya jamii), na toka Sh. bilioni 3,532.7 hadi Sh. bilioni 3,829.6 (usalama na utekelezaji sheria). Serikali iliahidi kutenga fedha kwa ajili ya masuala mtambuka, na hasa kwa kutaja utekelezaji wa MTAKUWWA[12] miongoni mwa malengo yake.

*Kwa mwaka wa tano, hakuna fedha maalum ziliozotengwa kwa ajaili ya afua au maeneo ya MTAKUWWA zilizoripotiwa na serikali.*

## Mapungufu Yaliyoainishwa

Utekelezaji wa ufadhili wa MTAKUWWA umekumbana na changamoto mbalimbali za msingi katika Wizara, Idara na Taasisi na pia Serikali za Mitaa zikijumuisha:

- Kutengwa kwa bajeti isiyokidhi mahitaji katika Wizara za kisekta, Tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zenye kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa MTAKUWWA.
- MTAKUWWA unakosa mfumo au mwongozo kwa ushiriki wa wadau hasa kutoka sekta binafsi kuhusu namna wanavyoweza kushiriki kusaidia utekelezaji wake.
- Kuendelea kuwapo kwa mila na desturi potofu na zenye madhara zinazoendelezwa na jamii bila kukemewa na mamlaka za serikali za mitaa.
- Upungufu wa wataalamu katika ngazi ya Wizara wanaoweza kuongoza utekelezaji wa maeneo ya kimkakati yaliyoainishwa kwenye MTAKUWWA, na pia ujuzi usiotosheleza kwa watumishi walio na jukumu la kuzuia na kushughulikia matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika ngazi ya serikali za mitaa.
- Mifumo dhaifu ya uwajibikaji, kufuatilia mienendo na mwelekeo wa utekelezaji wa MTAKUWWA unaosababishwa na kukosekana kwa mfumo ulio wazi na jumuishi wa kuripoti mafanikio na hatua zilizopigwa kwa kuzingatia viashiria vilivyopo katika mpango kazi.
- Kukosekana ulinganifu kati ya vipaumbele vya serikali na vile vya jamii hali inayotokana na mifumo dhaifu ya ushiriki wa jamii, kama vile ule wa Vikwazo na Fursa kwa Maendeleo (O&OD) kunaashiria ukosefu wa dira ya pamoja baina ya wadau katika kuwezesha na kufadhili utekelezaji wa MTAKUWWA.

12 Wizara ya Fedha na Mipango [2021] Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Dodoma, uk.50

## Hitimisho na Mapendekezo

Ingawa Serikali ya Tanzania imefanya jitihada kubwa katika kufadhili namna ya kushughulikia matukio katika ngazi ya taifa na wilaya, katika sura ya vipaumbele shindani vya kitaifa vinavyofungamanishwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, utengaji fedha katika bajeti umeendelea kuwa finyu. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inayosimamia idara zenye majukumu ya moja kwa moja katika ulinzi wa mtoto, mara kwa mara, imekuwa ikipokea chini ya 15% ya bajeti yote ya taifa katika kipindi ambacho mapitio haya yamefanyika. Hali hii husababisha ugumu katika kuwezesha afua muhimu. Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI zimekuwa zikipokea kiasi kidogo cha fedha hali inayoleta ugumu katika kuratibu kwa ufanisi na kuziwajibisha wizara nyingine pamoja na mamlaka za serikali za mitaa katika kutimiza malengo yaliyowekwa na MTAKUWWA.

Kwa kuzingatia mwenendo wa ufadhili, mapungufu na mafunzo yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti kwa miaka minne iliyopita, ripoti fupi hii inawasilisha mapendekezo yanayohusu sera, uratibu na utengaji bajeti kama ifuatavyo:

- Kutekeleza afua za kisera kwa ufanisi, ni vyema kutumia mfumo na muundo wa ngazi ya juu wa uratibu ili kuepusha athari zinazohusiana na kukosekana kwa ufanisi na mwingiliano wa mikakati kama ilivyoshuhudiwa katika utekelezaji wa mipango kazi minane (8) iliyopita.
- Kurejea na kufanya mapitio ya majukumu ya wadau wa ngazi za chini ili kuwezesha utekelezaji wa MTAKUWWA kupitia Kamati za Maendeleo za Kata na Kamati za Maendeleo za Vijiji ili kuhakikisha kunakuwa na urahisi na gharama nafuu kwa kamati za MTAKUWWA.
- Kuwezesha mbinu jumuishi za ushiriki wa wananchi katika kuandaa ajenda na michakato ya kibajeti inayohusu MTAKUWWA kwa kuzingatia na kuweka vipaumbele katika afua mahususi.
- Kushawishi ongezeko la bajeti inayotengwa na kupelekwa kwa fedha katika Idara ya Maendeleo ya Jamii kama mtekelezaji mkuu katika ngazi ya Wizara ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kutekeleza majukumu yake katika masuala yote yanayomhusu mtoto nchini.
- Kuongeza msaada na ushiriki wa AZAKI ili kuendeleza na kuimarisha hatua zilizochukuliwa katika ngazi za taifa na chini ili kuepusha na kudhibiti ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Ushiriki huo unatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kusimamia masuala haya.
- TAMISEMI inatakiwa kutengeneza miongozo ya wazi na kutoa maelekezo kwa uongozi wa mabaraza ya halmashauri kutenga bajeti maalumu katika mamlaka yao kwa ajili ya utekelezaji wa MTAKUWWA.
- Miongozo ya kibajeti inapaswa kutolewa ili kuhakikisha kila wizara husika inatenga fedha ili kuwezesha utekelezaji wa eneo la kimkakati wanaloliratibu au kulisimamia.
- Kufanya mapitio na kutengeneza mkakati stahiki unaoaminika na kutekelezeka wa kutafuta rasilimali na kuhakikisha kunakuwa na uwazi katika kufuatilia na kuripoti fedha zilizotengwa na kutumika kutekeleza shughuli zilizoainishwa katika maeneo mbalimbali ya kimkakati ya MTAKUWWA kwa kuwa na mafungu madogo maalumu katika bajeti.

Sweden Sverige

TGNP

In partnership with Canada

## Kwa Taarifa Zaidi


**Mtandao wa Jinsia Tanzania**
Mabibo Dar es saalam
S.L.P 8921
**Simu:** +255 754 784 050
**Barua Pepe:** info@tgnp.or.tz
**Tovuti:** www.tgnp.or.tz

@tgnptz1 @tgnptz @tvtapo

Tanzania Gender Networking Programme (TGNP)